



# PHARMACEUTICAL SOCIETY OF TANZANIA



P.O. Box 55666  
Dar-es-Salaam, Tanzania.



Tel:  
+255 754 942 678



Email  
[info@pst.or.tz](mailto:info@pst.or.tz)

Kumb Na AGM/RUH/2023/01

3 Agosti, 2023

Katibu Mkuu,  
Wizara ya Afya,  
S.L.P 743,  
Dodoma

YAH: RUHUSA KUHUDHURIA KONGAMANO LA SAYANSI NA MKUTANO MKUU WA CHAMA CHA WAFAMASIA TANZANIA, UTAKAOFANYIKA TAREHE 22 - 24 NOVEMBA 2023 KATIKA UKUMBI WA JAKAYA KIKWETE- DODOMA

Rejea Kichwa cha habari hapo juu,

Chama Cha Wafamasia Tanzania, (*Tanzania Pharmaceutical Society (PST)*), ni taasisi ilioanzishwa kwa lengo la kushirikiana na serikali na wadau mbalimbali ili kuwaleta pamoa wanataluma wa kada ya Famasi na kuenteleza taaluma, kuchoecha maadili bora ya utendaji kazi, kutoa mafunzo endelevu na kuchangia kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza.

PST imeshirikiana na Kitengo cha Huduma za Dawa Wizara ya Afya(PSU), Baraza la Famasi(PC), Mamlaka ya Dawa na vifaa tiba(TMDA), Bohari ya dawa(MSD), OR-TAMISEMI na wadau wengine kuandaa Kongamano la Sayansi kwa wataalamu wa kada ya famasi na wadau wa huduma za kifamasia nchini. Kongamano hili litafanyika tarehe 22 - 24 Novemba, 2023, katika ukumbi wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.

Kutakua na mada mtambuka kwa wataalamu wote wa kada ya famasi katika suala la ubora wa huduma, maadili, mbinu bora za usimamizi wa dawa na vifaa tiba, kuwafahamisha/kuwakumbusha juu ya sheria, kanuni na miongozi ya kada ya famasi. Tunatarajia kongamano hili kutumika kufikisha ujumbe mahususi kwa wataalamu wa kada ya famasi na wadau wake wote kwa mustakabali wa taifa.

Ili kufanikisha kongamano hili muhimu, tunakuomba uelekeze taasisi zilizo chini ya Wizara yako, kuwafahamisha na **kuwaruhusu** wanataluma wote wa kada ya Famasi katika taasisi hizo kuhudhuria kongamano hili.

Aidha kila mwanataluma anatakiwa kulipia Ada ya kongamano kama ifuatavyo: (**Angalizo:** Ada hii haihusishi gharama za usafiri na malazi)

Kundi	Ada ya Kongamano	Jumla
Mfamasia	100,000/=	100,000/=
Fundi Dawa Sanifu/Wasaki	50,000/=	50,000/=

Kwa barua hii PST inaomba, kwa taratibu za taasisi husika, wanataluma wa kada ya famasi wawezeshwe ada husika hapo juu. Pamoja na barua hii, tunafanya rejea katika waraka kumbukumbu namba **HB.472/566/01/111** wa Katibu Mkuu OR-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, unaolekeza waajiri kuwaruhusu wanataluma kushiriki mikutano ya vyama nya taaluma.

Malipo yote yafanyike katika akaunti ya chama kama iliyobainishwa hapa chini:

Jina la Akaunti: **The Pharmaceutical Society of Tanzania**

Namba ya Account: **23910001642**

Benki: **National Microfinance Bank – Oyster Plaza Branch**

Kwa taarifa, uthibitisho wa malipo na maulizo tafadhali wasiliana na mwenyekiti wa kamati ya maandalizi kwa namba 0754942678 a barua pepe [president@pst.or.tz](mailto:president@pst.or.tz)

Wako katika uboreshaji huduma za kifamasia Tanzania.

Fadhili Hezekiah  
Rais PST

## EXECUTIVE

### President

Fadhili Hezekiah.

### General Secretary

Benson Katundu.